# LBE 2009 – Migration

# Episode 6: Successful Africans in Germany

**Author: Daniel Pelz**

**Editor: Thomas Mösch**

**Translator: ---**

**------------------------------------------------------------------------**

## Characters:

**1 Narrator**, male or female
**5 voice overs:**

- **Petra Molnar**, female, mid-forties
- **Tumenta Kennedy**, male, 33 years
- **Florah Ikaya-Witte**, female, 29 years
- **Patrick Mahassen**, male, early fifties
- **Jan Witte**, male, early thirties

---

### Intro

Hujambo na karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu uhamiaji kati ya Afrika na Ulaya. Leo hii tunakutana nao Tumenta na Florence, Waafrika wawili waliokuja Ujerumani muda mrefu kidogo. Wote wawili wamefaulu katika maisha yao hapa Ujerumani. Je waliwezaje kufaulu? Iwapo unataka kupata jawabu basi kaa nasi ili usikie hadithi zao.

---

## Scene 1

1. **Soundclip Petra Molnar (German)**

   **"Ninafuraha kuwatambulisha kwa Tumenta, ambae atatufunza kwa leo. Miaka michache iliyopita alikuwa mwanafunzi kama ninyi lakini sasa anafanya kazi na taasisi inayohusika na maswala ya maadili ulimwenguni."**

2. **Narrator:**

   Kila jina lake linapotajwa mbele ya watu namna hii, Tumenta Kennedy anatambua ni hatua zipi alizopitia hadi kufikia hapa. Masikio na macho ya wanafunzi kutoka Afrika na Asia yote yanamulekea yeye. Wanafunzi wamevaa jeans na T-Shati wananukuu kwenye madaftari yao. Miaka miwili iliyopita kijana huyo alikuwa kama wao. Lakini leo mambo ni tofauti.

3. **Soundclip Tumenta Kennedy (German)**
   **„Jina langu ni Tumenta Kennedy. Kwa bahati mbaya sikupata fursa ya kupata kozi ya lugha ya Kijerumani. Nitagawanya mhadhara wangu katika sehemu tatu...** – *not audible in insert***)"**

4. **Narrator:**

   Leo, Tumenta Kennedy amevaa suti nyeusi, shati jeupe na miwani. Anaonekana kama meneja wa Benki. Yeye ni msimamizi wa mradi katika kituo cha Wittenberg kinachohusika na maswala ya maadili ulimwenguni. Taasisi ya Kijerumani inayotoa ushauri kwa mashirika ya serikali na sekta binafsi, pia ushauri kuhusu vipi jamii inavyoweza kufaidika na mienendo ya mashirika hayo. Leo hii amealikwa kuendesha warsha katika kituo hiki cha wanafunzi wa kigeni kilichopo Halle, Ujerumani Mashariki.

**Scene 2:**

5. **SFX Typing**

6. **Narrator:**

   Kilomita 180, kaskazini mashariki mwa Berlin, mji mkuu wa Ujerumani, Florah Ikaya-Witte ameianza siku yake kwa utaratibu. Amekaa ofisini mwake katika makao makuu ya Shirika la Kimataifa la Transparency International, jumuiya isiyo ya kiserikali ya kupambana na rushwa. Florah anaandika pendekezo kuhusu msaada.

   Kuna meza tatu za kawaida zilizo karibu karibu, rafu la mbao na karatasi la tangazo ukutani linaloonyesha picha ya mkono unaomkandamiza hakimu ardhini – ni kukumbushia harakati za vita dhidi ya rushwa katika maswala ya sheria huko Ulaya ya Mashariki. Florah Ikaya-Witte aliondoka nchini kwake Kenya mnamo mwaka 2005.

7. **Soundclip Florah Ikaya-Witte (English)**
   **"Mimi ni mtu ninaependa kufaulu, ninataka kufaulu popote pale nilipo kwa hivyo kila mara nitatafuta njia za kulifanikisha hilo, kwa sababu naamini kuwa mimi nina ujuzi unaoweza kunipa kazi, lakini kufikia hapa haikuwa rahisi pia, ingawa lazima niseme kuwa kazi hiyo ngumu imezaa matunda."**

**Scene 3:**

8. **SFX: Video Tumenta in Cameroon**

9. **Narrator:**
   Akiwa ofini mwake katika ofisi za kituo cha Wittenberg kinachohusika na maswala ya maadili ulimwenguni, Tumenta Kennedy anaonyesha video kwenye kompyuta yake. Aliinasa wakati wa safari yake ya hivi karibuni huko

nchini Cameroon. Video hiyo inaonyesha baadhi ya sababu zinazowafanya Waafrika wengi kupigania fursa ya kuja kuishi Ujerumani – na wengine kama yeye na Florah Ikaya-Witte kuishia katika nafasi za juu.

Kwenye video hiyo, anaonekana akiwa amesimama kwenye roshani. Chini yake kuna wimbi la wanafunzi kutoka shule za msingi wakiwa wamevalia sare zao za shule za rangi ya kahawia na nyeupe, wamesimama pamoja tayari kabisa kumsikiliza akieleza "siri ya mafanikio yake".

**10. Soundclip Tumenta Kennedy (English)**

**"Kilichotokea ni kwamba niliifahamisha familia yangu kuwa nisingeweza kuwapigia simu kila siku, kwa sababu gharama ni kubwa mno. Sikuweza kuwatumia fedha kila wiki au kila siku kwa sababu ningelazimika kufanya kitu ambacho ni kinyume cha sheria. Labda ningejihusisha na biashara ya madawa ya kulevya, au kama ningekuwa mwanamke labda ningejiingiza kwenye ukahaba ili niweze kutimiza mahitaji ya familia yangu."**

**11. Narrator:**

Lakini badala yake, Tumenta alitumia wakati wake na bidii kubwa kujifunza Kijerumani – kipengele cha muhimu kinacho mlazimu mtu akitaka kufaulu nchini Ujerumani. Jambo lingine ambalo lilikuwa la muhimu sana kwake, ilikuwa ni elimu yake ya chuo kikuu. Badala ya kufanya bidii kutafuta fedha za kupeleka nyumbani kwa familia yake, yeye alitilia mkazo elimu yake katika chuo kikuu na mwishowe akapata shahada yake.

**<u>Scene 4:</u>**

**12. Soundclip (English)**

**a) Patrick Mahassen**

**"Florah, ingiaa, unataka nini?"**

**b) Florah Ikaya-Witte**

**"Nilitaka tu kujua ni lini mkutano wetu utafanyika tena, kwa sababu leo haukufanyika."**

**13. Narrator:**

Lakini hakuna mtu anaejua ni kwa nini wao wamefaulu zaidi kuliko wakuu wao. Patrick Mahassen ni mkuu wa kitengo cha michango cha shirika la kimataifa la Transparency International. Ni mtu mchangamfu na ndio kwanza yumo mwanzoni mwa miaka 50, ana mvi na mara nyingi yeye huwa anatabasamu. Aliamua kumuajiri Florah kati ya zaidi ya watu mia moja walioomba nafasi hiyo. Patrick Mahassen hajawahi kusomea chuo kikuu katika maisha yake – alianza kama mwimbaji wa muziki wa rock, na baadae akajiunga katika kazi za maendeleo. Lakini hawezi kumshauri mtu yeyote kufuata njia yake hiyo.

**14. Soundclip Patrick Mahassen (English)**

**"Tunacho hitaji kutoka kwa watu wanaotoka Afrika, kwanza wawe ni watu wanao fahamu jinsi rushwa inavyotendeka na pia kufahamu kuwa rushwa ni kitendo kinachorudisha nyuma maendeleo. Wawe na elimu inayowawezesha kufanya kazi kwenye ofisi yenye majukumu na ushindani mkubwa. Elimu ya juu, inahitajika shahada ya uzamili lakini kwa Florah, kitu cha kuvutia zaidi ni uzoefu wake katika kazi za maendeleo nyanjani."**

**<u>Scene 5:</u>**

**15. SFX Video**

**16. Narrator:**

Tumenta Kennedy bado yupo ofisini, vitabu vimejazana kwenye rafu na mezani pake. Vitabu kuhusu maswala ya kila aina. Kwa mfano kitabu kuhusu "Ubepari wa mageuzi" "Creative Capitalism" kipo karibu na kitabu kilichoandikwa na baba mtakatifu Benedict wa 16 kinachoitwa "The Salt of the Earth" "Chumvi ya Dunia". Ukutani karatasi kubwa lenye majina ya wabunge wote wa Ujerumani linaning'inia. Mchanganyiko huu ni mfano mwingine wa mambo yanayompendeza Tumenta Kennedy. Kutoka elimu ya dini hadi Uchumi na biashara na pia kutoka kwenye maswala ya siasa hadi utamaduni wa Kiafrika. Watu wengi wanasema watu kama yeye wanadhuru maendeleo ya Afrika, kwa sababu wanaishi Ulaya, badala ya kutumia ujuzi wao kwa ajili ya maendeleo ya Afrika. Hakubaliani na lawama hizo hata kidogo.

**17. Soundclip Tumenta Kennedy (English)**

**"Ninawasaidia wanaopitisha maamuzi kuelewa, kwamba maswala ya soko huria hayahusiani na ufunguzi wa mipaka, lakini yanawasaidia watu wa nchi zao kushiriki katika ushindani wa kibiashara. Kwa hiyo kwenye hali hii, kazi yangu ni kuwa mtu wa kati: Ninatumia ufahamu ninaoupata kutokana na utafiti ninaofanya huko Afrika na kuwaelimisha watu wa Ulaya juu ya Afrika na wakati huo huo ujuzi ninaoupata Ulaya nautumia kujadiliana na Waafrika.**

**<u>Scene 6:</u>**

**18. SFX: Karabiner (dann darunter legen)**

**19. Narrator:**

Florah Ikaya-Witte hafanyi kazi leo. Jua linawaka mawinguni, miti yote imefunikwa na majani ya rangi kijani. Ni siku nzuri ya kupumzika nyumbani

huko Berlin. Akiwa pamoja na mumewe Mjerumani Jan, ambae ni daktari, ameamua kufurahia hali nzuri ya hewa leo hii.

**Atmo kurz hochziehen**

20. **Narrator:**

Wamesimama mbele ya ukuta mkubwa uliojengwa kwa zege, uliotumika kama kizuizi wakati wa vita. Watu wanaotaka kujaribu ujuzi wao wa kupanda wanaruhusiwa. Florah anamfunga mumewe kamba kwenye lupu ya mkanda wake huku akiwa anapanda polepole, kwa uangalifu anakanyaga kwenye sehemu zilizo na mwanya, Flora naye anashikilia kamba ile kuhakikisha usalama wa mumewe. Hatua hiyo itamzuia kuumia iwapo atateleza na kudondoka chini. Florah anasema kuwa amepata marafiki wengi katika jamii hiyo ya wapenda kupanda. Na hiyo ni sababu moja inayomfanya ajihisi kuwa yuko nyumbani hapa nchini Ujerumani.

**21. Soundclip Florah Ikaya-Witte (English)**

**"Kwa ajili ya kupata afueni ukiwa kwenye hali yoyote ile. Sisi sote ni binadamu, je ukiishi kwenye kisiwa nani atakusaidia iwapo utapata matatizo? Lazima uwe na rafiki ndio upate kuvuka, kwa hivyo lazima utoke. Ninawaona waafrika wenzangu wengi ambao wanakutana na watu wawili au watatu ambao wanawafahamu vyema tena waafrika wenzao tu; hawataki kuvuka mipaka yao. Lakini ukitaka kupata marafiki, kuishi maisha mazuri basi lazima utoke ukutane na watu mahala popote pale unapoishi."**

**22. Narrator:**

Na mtu ambaye amemzowea sana maishani mwake ni mumewe Jan. Walikutana katiika mji mkuu wa Kenya, Nairobi miaka mitano iliyopita wakati

Jan alipokuwa akifanya kazi ya kujitolea kwenye mradi wa watu wanoishi na virusi na UKIMWI nchini humo. Inakaribia miaka miwili sasa tangu walipooana. Watu wengine wanaweza kufikiri kuwa mke wake anaishi maisha ambayo ni ndoto ya wanawake wengi wa Kiafrika, yaani ndoto ya kuolewa na mtu mweupe. Lakini Jan anasema kuwa rangi ya ngozi sio swala katika ndoa.

**23. Soundclip Jan Witte (English)**

**"lazima kwanza ujihisi kuwa uko karibu sana na mtu anaetoka katika sehemu nyingine ya ulimwengu, hili ni jambo la muhimu sana. Hivi ndivyo ndoa au urafiki utakavyoweza kufana, hata kama watu hao wanatoka katika sehemu tofauti za ulimwengu. Binafsi, sijali ni wapi mwenzangu anakotoka lakini ninajali yeye mwenyewe ni mtu wa aina gani na kama ninaweza kuishi na mtu huyo, je tunaweza kuwa pamoja maishani, au kama ninaweza kuzungumza na mtu huyo tuelewane au tushindane kidogo. Hayo ndio maswala muhimu kwangu, si maswala ya tamaduni yanayofanya mapenzi kunawiri."**

**<u>Scene 7:</u>**

**24. SFX: Glocken**

**25. Narrator:**

Baada ya kazi, Tumenta Kennedy hupendelea kutemebea kwenye barabara zilizojengwa kwa mapande ya mawe kati kati ya mji wa Wittenberg. Anaupenda mji huo mdogo. Muhudumu wa kike katika mkahawa anamsalimia kwa tabasamu wakati anapita karibu na mkahawa huo. Mara anasimama kuzungumza kidogo na rafiki yake. Lakini Tumenta Kennedy anaupenda mji mdogo wa Wittenberg kwa sababu nyingine kabisa: Kwake, mji huu wa kihistoria una mafunzo mengi ambayo anaona kuwa yanaweza kuwa majibu kwa changamoto zinazolikabili bara la Afrika wakati huu. Tumenta Kennedy

anaelekea katika kanisa la Castle. Ni hapa ambapo inasemekana kuwa Martin Luther aligonga tasnifu zake 95 kwenye lango, ambazo zilikosoa sana kanisa Katoliki. Baada ya hapo kanisa la Kiprotestanti likazaliwa.

**26. Soundclip: Tumenta Kennedy (English)**

**"Nadhani Afrika sote tuna maadili ya kimsingi ya pamoja na kwamba kuishi pamoja kwa amani baina ya Waprotestanti na Wakatoliki kulitokana na mabadiliko katika kigezo cha fikra na kigezo cha mtazamo, ambapo Wajerumani hawakuwaona Wakatoliki na Waprotestanti kuwa ni maadui. Kwa hiyo barani Afrika ambako tunashuhudia mapigano kati ya makabila, ambapo kuna Wakristo na Waislamu katika familia moja na watu wengine wanaoamini madhehebu ya kiinjili inadhirisha, tunaweza kuishi kwa amani pamoja."**

**27. Narrator:**

Hii huenda ikawa ni sehemu nyingine ya ujuzi alioupata Tumenta Kennedy ambayo angependa kuchangia barani Afrika – kueleza wazi kwamba anaweza pia kuchangia katika maendeleo ya Afrika ijapokuwa yupo maelfu ya kilomita mbali na bara hilo.

**-------------------------------------------------------**

**Outro:**

Na hayo ndio tuliyoweza kukuletea kwa leo katika Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu Uhamiaji. Mwandishi wetu leo hii alikuwa ni Daniel Pelz. Iwapo ungependa kufahamu zaidi juu ya makala hii au makala zingine za Noa Bongo Jenga maisha Yako au pia kukisikiliza tena kipindi hiki. Tembelea kwenye mtandao wetu. Anuani yetu ni: www.dw-world.de/lbe Asante kwa kuwa nasi, hadi wakati mwingine. Kwaheri.